


Mtumishi wa Mungu: Eng John Ndindwa,
Huduma: Tag Shekina – Tabora
Somo: Mbegu
Email: ndindwajohn@gmail.com | Cell: 0717 401 569



*Yeremia 2:21 Nami nalikuwa nimekupanda, mzabibu mwema sana, mbegu nzuri kabisa; umegeukaje, basi, kuwa mche usiofaa wa mzabibu - mwitu machoni pangu?*

Yeremia 2:21 Nami nalikuwa nimekupanda, mzabibu mwema sana, mbegu nzuri kabisa; umegeukaje, basi, kuwa mche usiofaa wa mzabibu - mwitu machoni pangu?

Tafsiri ama maana

- Maana ya 1: Ni kitu chochote kinachokuwa na uhai toka kwa Mungu ili kuzalisha viumbe wengine kusudiwa na Mungu wanaofanana na Mungu.
- Maana 2: Ni mtu yoyote aliyeokoka anayefanyika kuwa uzao wa ADAM 2…
- Maana 3: Ni neno la Mungu ambalo huweza kuzaa: Luka 8:11 Ishu ya mpanzi na Udongo.. Injili ya neno la Mungu ni Mbegu inayoweza kuzaaa viumbe wa Mungu

ADAMU-1: Alikuwa ni kiumbe cha Mungu ambacho kilianzia Mbinguni (Ulimwengu wa roho mbinguni) ambacho baadae, kiligeuka mbegu kikaletwa duniani katika jimbo jipya la Mungu ili iwe chanzo cha kuzalisha viumbe wanaofanana na Mungu.

Viumbe wanaofanana na Mungu

Ni viumbe wataouishi ufalme wa mbinguni (nchi ya mbinguni) wao wakiwa jimbo la duniani. Duniani tuko katika mwili lakini kati ya wanaomwamini Mungu na wasiomwamini kuna ukuta mkubwa unaotenganisha nchi ya duniani na nchi ya mbinguni.

*Mwanzo 1:22 Mungu akavibarikia, akisema, Zaeni, mkaongezeke, mkayajaze maji ya baharini, ndege na wazidi katika nchi. Mwanzo 9:1 Mungu akambariki Nuhu na wanawe, akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi*

Mbegu hii ilikuwa na Tabia ya utakatifu ili itimize kusudi la Mungu. Dhambi ilipoingia kusudio hili likaharibika kwa sababu isingezaaa viumbe wanaofanana na Mungu.

ADAMU-2: Ndiye Mungu katika mwili alipitia jina la Adamu kwa sababu jina kusudiwa jimbo la duniani lilikuwa ni la Adamu. Lazima Mungu alitumia itifaki yake kuja duniani.

Utofauti wa nchi hizi mbili

| | ENEO HUSIKA | SERIKALI YA KIDUNIA | SERIKALI YA MBINGUNI |
|---|---|---|---|
| 1 | KATIBA NA UONGOZI WAKE | Ni mawazo ya watu wengi, Hutambua makosa na si dhambi, hawatambui utakatifu.<br>- Kitabu cha sheria ya nchi hakuna neno DHAMBI wala UOVU<br>- Uongozi wake ni Raisi, Makamu, na waziri Mkuu chini ya Serikali kuu, Mahakama na Bunge. | Ni wazo la Mungu pekee, hutambua Dhambi na utakatifu. Biblia ni kitabu cha Mungu cha kiagano.<br><br>Mfumo wake ni Mfalme, Kuhani na Nabii.<br>2 Nyak 7:14 |
| 2 | ULINZI | JWTZ \| POLISI | Jeshi la Mungu la malaika, Zab 34:7 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Wanatumia Bunduki, mabomu ya machozi, vifalu, | Watumia Maombi, wema, Injili, Neno la Mungu |
| **3** | KUIGEUZA JAMII | Mahakama, Jera, Mahabusu, Mateso (Hard power)<br>- Jera walio wengi ni masikini<br>- Wezi wakubwa wengi hawako<br>- si wote walifungwa waliiba | Injili pekee ya neno kweli la Mungu inapohubiriwa na watumishi itwa na sahihi watu wanaacha maovu na dhambi zao na tabia zao bila viboko wala mateso yoyote, (Soft Power |
| **4** | SIFA ZA VIONGOZI | Sehemu huangalia Elimu ya duniani | Ni kipawa cha Mungu na hekima itokayo kwa Mungu. Mdo 3:6 |
| **5** | IBADA | Hakuna kumwabudu Raisi | Kuna wajibu wa mbegu ya MUNGU kumwabudu Mungu. |
| **6** | UCHUMI | Kulima, viwanda, Nishati<br><br>- Mungu akiacha mvua hakuna kitu. | Sadaka za kweli kwa Mungu, Fungu la Kumi, Kujitoa, kusaidia na kumcha Mungu. |
| **7** | KUZIBEBA SHERIA NA KANUNI | Ni kupitia Training, Mafunzo, kuandika, Bunge na Mahakama. | Mungu huziweka ndani yetu. Yer 31:33 1 yoh 5:3 |

TABIA ZA MBEGU

1. Ina uhai ndani yake. Ambao huweza kutengeneza uzima wa viumbe wengine, inaweza
   1 Petro 1:23 Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.
   Ina uhai unaoonekana mara baada ya kufa. Ili uhai uonekane lazima ionekane kama imekufa. Yesu alipitia mchakato wa kufa mwili wake ili aweze kuwazaa na kuwaleta wanadamu katika sehemu ya adamu wa Kwanza.
   Mkristo lazima afe: ndio aokokoke kama akikataa kufa hawezi kuwa ameokoka.
   **Kuna mambo Mungu anangoja yafe ndipo ajifunue kwako:**
   - Tamaduni za zamani zife, Marafiki wa zamani wafe, Tabia za zamani kufa….Mfalme uzia alipokufa ndipo isaya alipomwona Bwana.
   - Ibrahimu alipoachana na Ruthu ndipo Mungu alipojifunua.
2. Inaweza ikaongezeka na kujijumlisha.
   - Kipawa kwa kipawa, Huduma na huduma, Neema hadi neema,
   - Lazima uzae watumishi wengine wenye huduma kama ya kwako, Waliokoka kwenu kama wewe,
   - Unaweza ukawa na kipawa zaidi ya kimoja, Huduma zaidi ya moja maana ni yeye Yule na humpa mtu mwenye kiu ya kumtumikia Mungu.
   - RM alikuja kuhakikisha kazi ya Mungu inasambaa kila mahali na ndivyo ilivyo ndani ya watu wake ama kanisa.
3. Inaweza kuchukua nafasi, Ama ina tawala. Ulimwengu wa roho. Inapoongezeaka lazima ichukue nafasi Fulani. Kazi ya ujio wa RM kuja kuhakikisha injili inahubiriwa na falme za giza zinaangushwa mahali mbali mbali.
   Luka 10:19 Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.

   **Usikose Sehemu ya Pili**